**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**03 MAARIFA YA JAMII**

**Muda: Saa 1:30** **MAJIBU** **Mwaka: 2020**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali manne (4).
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.

maktaba.tetea.org

TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

SEHEMU A (Alama 28)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Jibu kipengele cha (i) – (viii) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika katika kisanduku.

(i) Kwanini kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania?

A. Kinapendwa na watu wengi

B. Kinavutia watalii wengi

C. Kinaajiri watu wengi

D. Kinavutia uchimbaji wa madini

**C. Kinaajiri watu wengi**

Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi kwa sababu **kimeajiri idadi kubwa ya Watanzania na kuwa chanzo kikuu cha kipato kwa wananchi wengi**.

(ii) Nchi ya Tanzania inafaidika vipi na uchimbaji wa madini?

A. Kupata fedha za kigeni

B. Kuongezeka kwa mazao

C. Kuongezeka kwa mifugo

D. Kuongezeka kwa misitu

**A. Kupata fedha za kigeni**

Uchimbaji wa madini huingizia nchi **fedha za kigeni kupitia mauzo ya madini nje ya nchi**.

(iii) Ni athari ipi ya uharibifu wa mazingira haisababishwi na uchimbaji wa madini?

A. Ukataji wa miti hovyo

B. Ongezeko la mvua

C. Uchafuzi wa maji

D. Kuwepo mashimo makubwa


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

**B. Ongezeko la mvua**

Ongezeko la mvua **halisababishwi na uchimbaji wa madini**, bali ni jambo la kiasili la hali ya hewa.

(iv) Ipi ni faida ya mbuga za wanyama nchini Tanzania?

A. Kuongeza pato la Taifa

B. Kupata samadi ya kilimo

C. Kuongezeka kwa uwindaji haramu

D. Kupata ardhi nzuri ya kilimo

**A. Kuongeza pato la Taifa**

Mbuga za wanyama **huvutia watalii wanaoingiza fedha na hivyo kuongeza pato la Taifa**.

(v) Ni kwa nini matumizi ya baruti na sumu hayakubaliki katika shughuli za uvuvi?

A. Huua samaki wengi kwa wakati mmoja

B. Huwapa wavuvi hasara kubwa

C. Hunasa samaki wakubwa tu

D. Husababisha wavuvi kukosa ajira

**A. Huua samaki wengi kwa wakati mmoja**

Baruti na sumu **huua samaki wadogo na wakubwa bila kuchagua na kuharibu mazalia ya samaki**.

(vi) Ni madini yapi yanapatikana nchini Tanzania tu?

A. Tanzanaiti

B. Dhahabu

C. Almasi

D. Chokaa

**A. Tanzanaiti**

Tanzanaiti ni **madini adimu yanayopatikana Tanzania pekee duniani**.

(vii) Nini kifanyike ili kurekebisha eneo lililoathiriwa na shughuli za uchimbaji wa madini?

A. Kufuga mifugo wengi

B. Kusafisha ardhi

C. Kumwagilia maji

D. Kupanda miti

**D. Kupanda miti**

Kupanda miti **hurejesha uoto wa asili na kusaidia kurekebisha mazingira yaliyoharibika**.

(viii) Ni fursa ipi ya uchumi inayotokana na misitu?

A. Uzalishaji wa nafaka

B. Shughuli za uvuvi

C. Shughuli za ufugaji nyuki na urinaji asali

D. Uchimbaji wa madini

**C. Shughuli za ufugaji nyuki na urinaji asali**

Misitu **hutoa fursa za ufugaji nyuki na uzalishaji wa asali ambao ni chanzo cha kipato**.

2. Jibu kipengele cha (i) – (vi) kwa kuoanisha maelezo ya vifaa vinavyotumika kupima hali ya hewa katika Fungu A na majina ya vifaa husika katika Fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

(i) Kifaa kinachotumika kupima uelekeo wa upepo

**B. Kampbeli stok**


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

(ii) Kifaa kinachotumika kupima unyevuanga

**A. Haigromita**

(iii) Kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa

**G. Baromita**

(iv) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi

**C. Kipimajoto**

(v) Kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo

**F. Anemomita**

(vi) Kifaa kinachotumika kupima mwanga wa jua

**H. Stevenson screen**

SEHEMU B (Alama 22)

3. Soma majadiliano yafuatayo kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Dihenga: Hujambo?

Masatu: Sijambo.

Dihenga: Hivi wewe ni kabila gani?

Masatu: Mimi ni Msukuma, wewe je?

Dihenga: Mimi ni Mzaramo.

Masatu: Nimesikia jana ulikuwa unacheza ngoma katika sherehe

Dihenga: Ndiyo tulikuwa tunacheza ngoma iitwayo mdundiko. Wewe hupendelea ngoma gani?

Masatu: Na mimi pia napenda mdundiko kwa sababu mwili unakuwa imara

Dihenga: Je unapendelea kusalimia watu katika jamii yako?

Masatu: Ndiyo mara nyingi ninasalimia watu mbalimbali katika jamii yangu.

Dihenga: Mnasalimianaje katika jamii yako?

Masatu: Tunasalimiana kwa kushikana mikono, wewe je?

Dihenga: Mimi napenda kusalimiana kwa kukumbatiana.

Masatu: Ooh! Hongera.

Dihenga: Ahsante.

**Maswali:**

(i) Masatu ni kabila gani?

Masatu ni Msukuma.

(ii) Dihenga hupendelea kusalimianaje?

Dihenga hupendelea kusalimiana kwa kukumbatiana.

(iii) Taja aina ya ngoma wanayocheza Wazaramo.

Wazaramo hucheza ngoma ya mdundiko.

(iv) Kwa mujibu wa majadiliano hayo, ni kabila gani husalimiana kwa kushikana mikono?

Ni Wasukuma.

(v) Taja faida ya kucheza ngoma ya "mdundiko".

Faida yake ni kuufanya mwili uwe imara na wenye afya.

(vi) Mazungumzo kati ya Masatu na Dihenga yalianzaje?

Mazungumzo yalianza kwa salamu "Hujambo?".

(vii) Umejifunza nini kutokana na majadiliano hayo?

Nimejifunza kuthamini tamaduni za makabila mbalimbali na umuhimu wa salamu katika jamii.

4. Je, alama zifuatazo zinawakilisha nini katika ramani?
    (i) Daraja
    (ii) Dira
    (iii) Mto
    (iv) Reli